

Alberta inaita wajuzi wa biashara.

May 01, 2024 [Maswali ya vyomba vyahabari](#)

Alberta inatoa wito kwa wafanyabiashara wenyewe ujuzi kusaidia kujaza nafasi muhimu kwenye soko la ajira la Alberta.

Alberta inaendelea kuongoza Canada kwenye uwekezaji na utengenezaji wa ajira. Wafanyakazi wa Alberta wanaendelea kuongoza kwa kulipwa pato la juu kwa juma kuzidi majimbo mengine, uwekezaji kwa kila mtu ni mkubwa Canada na pato halisi linakadiriwa kuzidi kiwango cha wastani cha taifa kwa asilimia 2.9 mwaka huu – kitu ambacho kinasaidia kuendesha ukuaji wa ajira. Kadri kazi nyingi zinavyotengenezwa, makampuni yanahitaji zaidi wafanyakazi wenyewe ujuzi ili kuendana na kasi.

Ili kusaidia kujaza nafasi muhimu za kazi katika biashara zenyewe ujuzi, serikali ya Alberta imezindua awamu ya tatu ya kampeni ya ‘Wito wa Alberta’ ambaao kwa sasa ipo kwenye soko la British Columbia, Quebec na Ontario. Kampeni hii inapewa nguvu na Bonasi ya Kuhama ya Wito wa Alberta – ambayo kwa mara moja ni mkopo wa kodi unaorejeshwa wa \$5,000 ikiwa na lengo la kuchochea wafanyakazi wenyewe ujuzi kuja Alberta kusaidia kujenga nyumba na miundombinu inayohitajika kuhimili jimbo linalokuwa.

“Uchumi wa Alberta unaoendelea kukua unawakilisha utajiri wa fursa za wafanyakazi wenyewe ujuzi kote nchini. Kampeni ya Wito wa Alberta na Bonasi ya Kuhama inathibitisha uthabiti wa serikali yetu katika kuvutia vipaji vya juu na kushughulikia mahitaji ya nguvu kazi katika sekta ambazo ni nyeti kwa kudumisha ustawi wa jimbo letu. Pia inaonesha kuwa tupo makini kwenye kujaza nafasi muhimu kwa kuweka wafanyakazi bora kusaidia mahitaji yanayoongezeka ya miundombinu.”

Matt Jones, Waziri wa Kazi, Uchumi na Biashara

Sekta za ujenzi wa makazi na usio wa makazi katika jimbo yanatarajiwa kuendelea kuongezeka kwa muongo ujao. Tathmini ya hivi karibuni kutoka BuildForce Canada

inaonesha Alberta itakuwa na ongezeko la ajira katika sekta ya ujenzi ya wafanyakazi 14,000 kati ya mwaka 2024 na 2033. Na kwa namna biashara ya kujenga nyumba ilivoanza kukua na kwa uwekezaji wa mabilioni ya dola uliofanywa kwenye jimbo, kama vile mradi wa Path2Zero kule Fort Saskatchewan, uhitaji wa wafanyakazi katika hiyo biashara unazidi kuwa mkubwa.

Kampeni itaangazia taaluma nyingi na manufaa ya mtindo wa maisha hapa Alberta, ikiwemo uwepo wa soko kubwa la ajira, mshahara mkubwa, kodi ndogo Canada, unaifuu wa makazi na uwepo wa jamii mbali mbali.

"Awamu ya tatu ya kampeni ya Wito wa Alberta ni kuweka mkazo kuhusu umuhimu wa wafanyakazi wenye ujuzi wa biashara kwenye uchumi wa Alberta na kwa ubaadae wetu. Kwa kifupi, tunawahitaji! Bonasi ya Kuhama inaakisi uwekezaji mkubwa kwenye elimu ya biashara ambayo tunaendelea kutoa kwenye bajeti yetu ya mwaka 2024. Kwa nyongeza, ni kitu kinachoonekana, chenye faida zinazosaidia kuchochea wafanyakazi wenye ujuzi kufanya maamuzi sahihi ya kuhamia Alberta."

Rajan Sawhney, Waziri wa Elimu ya Juu

"Biashara zenyе ujuzi za Alberta hutoa fursa nzuri za utaalamu. Jimbo letu linalekeea kupata ongezeko la kazi kuitia miradi kama vile Air Products na Dow. Kama unatafuta jimbo bora lisilokuwa na ukosefu wa kazi, basi huu ni muda mzuri wa kuja Alberta."

Terry Parker, Mkurugenzi Mkuu, Biashara ya Ujenzi wa Alberta

Bajeti ya mwaka 2024 imeelekeza kiasi cha \$10M kwa ajili ya Bonasi ya Kuhama ya Wito wa Alberta. Hii itasaidia wafanyakazi 2,000 katika biashara kuhamia Alberta na kugundua ni kwa nini ndio sehemu bora ya kuishi, kufanya kazi, kuwekeza na kulea familia. Vigezo vinavyohitajika vinapatikana kwenye tovuti ya Wito wa Alberta.

Mambo ya haraka

- Mwezi Agosti 2022, serikali ya Alberta ilizindua kampeni ya Wito wa Alberta kusaidia kutatua changamoto ya uhaba wa wafanyakazi.
 - Awamu ya 1, iliyoanza Agosti 2022, ilijikita katika kuvutia wafanyakazi wenye ujuzi kwenye sekta za huduma ya afya, biashara na teknolojia kutoka Toronto na Vancouver.

- Awamu ya 2, iliyoanza Machi 2023, ililenga mikoa ya Ontario na Atlantic Canada iliyokuwa na idadi kubwa ya watu wasiokuwa na ajira.
- Awamu ya 3, ambayo itaanza kazi Mei 1 mpaka Julai 2, 2024, imelenga wafanyakazi wenye ujuzi kwenye biashara kutoka British Columbia, Quebec na Ontario. Hii awamu itakuwa finyu zaidi kwenye muundo na itatumika kutangaza Bonasi ya Kuhama kwa watu wenye ujuzi wa biashara.
 - Awamu ya 3 ya kampeni inahusisha matangazo kwenye vyuo vikuu, migahawa, baa na maeneo ya mazoezi, redio, vyombo vyatuhusu na matangazo kwenye mitandao ya kijamii na tovuti iliyohuishwa ya Wito wa Alberta - AlbertaisCalling.ca
 - Awamu ya 3 ya kampeni inatarajiwa kugharimu kiasi cha \$2.5M.

Habari zinazohusiana

- [Wito wa Alberta](#)

Maswali ya vyombo vyatuhusu

[Josh Aldrich](#)

587-338-7509

Katibu wa Habari, Kazi, Uchumi na Biashara